#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo Na. 19

Julai - Septemba 2025



JAMBO LETU

Jaqueline Msuya
*Mhariri*

NDANI...



04
VIONGOZI WA ZHESLB WATEMBELEA HESLB



07
WIKI YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR



# WANAFUNZI ZAIDI YA 1,000 KUNUFAIKA NA 'SAMIA SCHOLARSHIP'

**DODOMA, JULAI 22, 2025**

Serikali imetangaza kuongeza idadi ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza watakaonufaika na mpango wa ufadhili wa masomo kupitia 'Samia Scholarship' kwa mwaka wa masomo 2025/2026, ambapo jumla ya wanafunzi 1,051 wanatarajiwa kupata ufadhili huo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Julai 22, 2025, Jijini Dodoma, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alibainisha kuwa ongezeko hilo linatokana na bajeti iliyotengwa kwa mwaka huu ambayo imeongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita, ambapo wanafunzi 640 wa mwaka wa kwanza ndio walifadhiliwa.

"Kati ya wanafunzi hao, 51 ni wenye mahitaji maalum waliopata ufaulu wa daraja la kwanza katika masomo ya sayansi kwenye mtihani wa kidato cha sita (2025)," alieleza Prof. Mkenda, na kuongeza, "… wengine 1,000 ni waliopata ufaulu wa juu katika masomo hayo kitaifa."

Ufadhili huo unalenga maeneo ya kipaumbele ya TEHAMA, Hisabati, Elimu Tiba, Sayansi na Uhandisi.

Aidha, kati yao, wanafunzi 50 watafadhiliwa masomo nje ya nchi katika maeneo ya Akili Unde (Artificial Intelligence), sayansi ya Data (Data Science) na masomo yanayohusiana na fani hizo ambao pia watapaswa kuomba kupitia mpango maalum wa Samia Extended Scholarship AI/DS/AI+.

Amebainisha kuwa majina ya wanafunzi wenye vigezo yanapatikana katika tovuti ya Wizara, www.moe.go.tz na ile ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; www.heslb.go.tz

Waziri Mkenda pia alibainisha kuwa wanafunzi watakaoomba ufadhili wa Samia Skolashipu Extended DS / AI + watapitia mafunzo ya miezi kumi katika kambi maalumu ya maarifa (Boot Camp) itakayowekwa katika Taasisi ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia iliyopo Arusha ili kuwaandaa vyema kujiunga na programu hizo pamoja na masuala mengine muhimu ukiwemo uzalendo kwa nchi yao.

Ufadhili wa 'Samia Scholarship' umeendelea kuwa chachu ya kuwainua vijana kitaaluma na kuwajengea uwezo katika sekta muhimu kwa maendeleo ya Taifa kulingana na Dira ya Taifa ya 2050.

# UREJESHAJI MIKOPO KUSHIRIKISHA WADAU WA KIMKAKATI



**DAR ES SALAAM, JULAI 01, 2025**

HESLB imeendelea kuwa moja ya taasisi zenye ufanisi mkubwa nchini hususan katika eneo la ugharimiaji wa wanafunzi katika ngazi ya vyuo vya elimu ya juu na vyuo vya kati na hivyo kuwa na uhakika wa mwendelezo wa kupata wataalamu wa sekta mbalimbali.

Pongezi nyingi kwa viongozi wa HESLB kwa jitihada za makusudi za utoaji elimu kwa wanufaika wa mikopo wa ndani ya nchi na wale walio nje ya nchi 'Diaspora' ambao mikopo yao imeiva na wameanza kurejesha bila shuruti.Sambamba na hilo, kampeni mbalimbali zimeendelea kufanyika zikiutaka umma wa watanzania kuwa na uzalendo ili kuendelea kuiimarisha taasisi hii inayotegemewa na watanzania katika kugharimia wanafunzi wahitaji kupata elimu ngazi ya kati na juu katika vyuo vinavyotambulika na mamlaka za ithibati ya elimu katika ngazi hizo mbili.

Baada ya pongezi hizo, turudi kwenye jambo letu, toleo hili limejikita katika kuongeza nguvu na ushirikiano wa kimkakati ili kuwafikia walionufaika na mikopo ya elimu ya juu waweze kurejesha mikopo hiyo iweze kuwanufaisha watanzania wengine wahitaji.

Hivi karibuni Menejimenti ya HESLB imeshiriki katika Tamasha la michezo (Serengeti Bonanza) lililofanyika katika Jiji la Antwerp- nchini Ubelgiji. Tamasha hilo limeshirikisha watanzania (Diaspora) wapatao 470 kutoka nchi za Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Sweden, Denmark, Uholanzi na nchi mwenyeji Ubelgiji.

Baadhi ya watanzania waliiohudhuria Serengeti Bonanza ni wanufaika wa Mikopo inayotolewa na HESLB ambao mikopo yao imeiva na wanarejesha kila mwezi kwa viwango tofauti tofauti.

Ni ukweli ulio wazi kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya uwekezaji mkubwa wa elimu katika kipengele cha utoaji wa mikopo ya elimu ya juu tangu mwaka 1994/1995 ambayo imewanufaisha watanzania zaidi ya 830,000 kwa kutumia zaidi ya TZS 8.2 Trilioni.

Kwa muktadha huo, HESLB inatoa wito kwa wadau wake kuendelea kuwa na uzalendo katika suala la urejeshaji mikopo ambapo fedha hizo zitawezesha wadogo zao ambao ni wahitaji kupata kusoma kwa kiwango cha elimu ya stashahada au shahada ili kutimiza ndoto zao.

Aidha, rai hii pia inaelekezwa kwa wadau wa elimu na maendeleo ya taifa letu waliopo ndani na nje ya nchi kuungana katika kutafuta mbinu za kuwabaini na kuwafikia wanufaika ambao hawajaanza kurejesha madeni yao yaliyoiva. Dawa ya deni ni kulipa.

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Dkt. Bill Kiwia

**Katibu**
Amani Kakana

**Mhariri**
Jaqueline Msuya

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Ramadhan Namaru

**Designer**
Abdul K. Msangi
+255 621 579 833

**Mawasiliano**
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**
+255 758 067 577
+255 739 067 577

**Barua pepe:**
info@heslb.go.tz

**Tovuti:**
www.heslb.go.tz


HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



## 2025/2026 utakuwa wa tija katika nyanja za kiutendaji, uwajibikaji na utoaji huduma kwa wateja

DAR ES SALAAM, JULAI 10, 2025
Nakukaribisha tena msomaji wetu katika toleo la 19 la Jarida hili la Mtandao ili kupata kwa muhtasari yaliyojiri HESLB ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku na pia matukio muhimu ya kitaifa yaliyofanyika katika sekta ya elimu katika robo ya kwanza ya mwaka 2025/2026.

HESLB ina matarajio makubwa kwamba mwaka huu wa fedha 2025/2026 utakuwa wa tija katika nyanja za kiutendaji, uwajibikaji na utoaji huduma kwa wateja ikiwa ni mwendelezo wa ufanisi wa kazi wa mwaka uliotangulia.

Mafanikio ya mwaka huu 2025/2026 ni mwendelezo wa mwaka 2024/2025 ambao ulikuwa wa mafanikio makubwa kwa HESLB na Serikali kwa ujumla katika kuhakikisha utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu unafanyika kwa ufanisi, na rahisi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA na kuzingatia miongozo ya kiutendaji.

Kipekee nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi na weledi wake wa kuidhinisha ongezeko la fedha kwa ajili ya kugharimia masomo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa mwaka 2025/2026. Hii inamaanisha wanafunzi wa Tanzania wana uhakika wa kusoma katika ngazi zote za elimu kwa ufadhili wa Serikali.

Shukrani pia kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda na Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB ikiongozwa na Profesa Hamisi Dihenga; chini ya uongozi wao, HESLB inazidi kuwa imara zaidi.

Mwaka 2025/2026, Serikali imeteenga TZS 917 bilioni kwa ajili ya bajeti ya kugharimia wanafunzi wa elimu ya juu; ambapo wanafunzi 88,320 ni wa mwaka wa kwanza (Freshers) na wanafunzi 164,453 ni wanaondelea na masomo (Continuing), hivyo kufanya jumla ya wanafunzi 252,773 wanatarajiwa kunufaika na mkopo wa elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2025/2026.


HESLB ikiwa miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), imepewa jukumu la kusimamia na kuhakikisha wanafunzi wahitaji wa Kitanzania wanagharimiwa masomo yao ya elimu ya juu katika fani mbambali.

Fedha zilizotengwa zitaongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka wanufaika 247,438 (2024/2025) hadi kufikia wanufaika 252,773 (2025/2026).

Aidha, Waziri Mkenda katika hotuba yake ya bajeti alibainisha kuwa Serikali itaendelea kutoa fursa za Elimu ya Juu kwa wanafunzi wenye ufaulu uliojipambanua kutoka wanafunzi 640 waliofadhiliwa mwaka 2025/2024 hadi wanafunzi zaidi ya 1,000 wanaotarajiwa kunufaika mwaka 2025/2026 kupitia 'Samia Scholarship' kwenye masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

Menejimenti ya HESLB imejipanga kuendelea kusimamia mikopo na 'Samia Scholarship' ya wanafunzi wa elimu ya juu kulingana na ustahiki wa wanafunzi wahitaji wanaolengwa kunufaika kwa kugharimiwa masomo yao kwa mwaka 2025/2026.

> *"Mafanikio ya mwaka huu 2025/2026 ni mwendelezo wa mwaka 2024/2025 ambao ulikuwa wa mafanikio makubwa kwa HESLB na Serikali kwa ujumla katika kuhakikisha utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu*



# Wahitimu 50 wapata ufadhili wa 'Samia Scholarship Extended' kusomea akili unde na ya Data

**Dar es salaam, Agosti 31, 2025**

Wahitimu 50 waliofanya vizuri katika masomo ya Sayansi kwenye matokeo ya Kidato cha Sita mwaka 2025 wamechaguliwa kupata ufadhili wa Samia Scholarship Extended, kusomea programu za Akili Unde, Sayansi ya Data na Sayansi Shirikishi katika vyuo vikuu mahiri duniani.

Taarifa hiyo imetolewa , Agosti 31, 2025 jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, ambaye amesema kuwa wahitimu waliochaguliwa wametokana na ufaulu wao bora katika tahasusi za PCM, PMC na PGM.

Prof. Nombo amesema kuwa wanafunzi hao watawekwa katika Kambi Maalumu ya Maarifa (Boot camp), ambapo watapatiwa mafunzo ya kujenga misingi katika matumizi ya kompyuta, programu na uchambuzi wa mifumo, pamoja na kusaidiwa kufanya maombi ya udahili katika vyuo vya nje ya nchi.

Ameeleza kuwa mafunzo hayo yatatolewa na wataalamu wabobezi kutoka ndani na nje ya nchi, wakiwemo kutoka sekta binafsi na diaspora, kwa kipindi cha miezi 10.

Aidha watapata fursa ya kufanya mitihani itakayowawezesha kupata vyeti vya kitaaluma mfano IBM, Certificate-Machine Learning for Data Science Projects, Certified Certificate in Cyber Security Standards na AWS Certified Cloud Practitioner vinavyotambulika kimataifa.

Ufadhili huu ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, toleo la 2023, inayolenga kutoa elimu inayozingatia ujuzi kulingana na soko la ajira na stadi za karne ya 21 ili kuchangia katika maendeleo ya Taifa na kimataifa




# DKT. BILL KIWIA AKABIDHI FEDHA ZA VIFAA VYA MAABARA SHULE YA SEKONDARI TEMEKE, HASNUU MAKAME ZANZIBAR

**Dar es Salaam & Zanzibar, Ijumaa, Septemba 16 & 17, 2025**

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imekabidhi kiasi cha Shilingi Milioni kumi (TZS 10,000,000) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara katika Shule ya Sekondari Temeke pamoja na Shule ya Sekondari Hasnuu Makame iliyopo Zanzibar, hatua ambayo inalenga kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuinua viwango vya ufaulu katika masomo ya sayansi.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, amesema msaada huo ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi iliyotolewa na taasisi hiyo wakati wa maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwake ambapo kupitia michango ya wadau, HESLB imeweza kutenga sehemu ya fedha kwa ajili ya kusaidia shule mbili za sekondari, moja ya Tanzania Bara na nyingine ya Zanzibar, kwa kuwapatia msaada wa fedha kwa ajili ya vifaa vya maabara.

"Pamoja na kuwa tunatimiza ahadi tuliyoitoa, msaada huu pia ni sehemu ya jitihada za HESLB katika kuunga mkono maendeleo ya sekta ya elimu, hususan masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM). Tunatambua kuwa taifa letu haliwezi kufikia uchumi wa kati wa viwanda bila kuwekeza katika elimu ya sayansi na teknolojia kuanzia ngazi za chini," amesema Dkt. Kiwia.

Akitoa neno la shukrani, Mkuu wa Shule ya Sekondari Temeke, Mwalimu Ingia Madika Mtenga, ametoa shukrani kwa Serikali, HESLB na wadau wote wa elimu kwa mchango huo, akieleza kuwa msaada huo utakuwa chachu ya mabadiliko makubwa kwa wanafunzi kwa kuwawezesha kujifunza kwa vitendo kwa ufanisi mkubwa.

"Fedha hizi zitasaidia kufanya maboresho makubwa na kununua vifaa muhimu vya maabara, jambo litakalowasaidia wanafunzi wetu kujifunza kwa vitendo na kuongeza ufaulu katika masomo ya sayansi," amesema Mwalimu Mtenga.

Akizungumzia vifaa vitakavyoongezwa katika maabara ya shule hiyo, Mwalimu Mtenga ameeleza kuwa wamepanga kununua vifaa vitakavyosaidia katika ufundishaji na kujifunza masomo ya Bailojia (Biology), Kemia (Chemistry) na Fizikia (Physics).

"Tunatambua jitihada za Serikali kupitia Bodi ya Mikopo kwa kuwawezesha wanafunzi katika elimu ya kati na ya juu. Fedha hizi tulizopokea leo zitasaidia kuongeza vifaa kama mashine za kuchuja maji na 'models' zinazoonyesha mfumo wa binadamu kwa maabara ya Baiolojia. Tunashukuru na tunaipongeza Serikali kupitia Bodi ya Mikopo, na tunamtakia kila heri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake katika kuimarisha sekta ya elimu," ameeleza Mwalimu Mtenga.

Kwa upande wa Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA), Dkt. Mwanakhamis Adam Ameir, ameongoza hafla ya makabidhiano ya TZS 10,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara katika Shule ya Sekondari Hasnuu Makame, Mkoa wa Kusini Unguja.

Akizungumza katika hafla hiyo Dkt. Mwanakhamis ameishukuru HESLB kwa msaada huo na kusisitiza umuhimu wa matumizi sahihi ya fedha hizo kwa manufaa ya wanafunzi na walimu.

"Naishukuru HESLB kwa msaada huu ambao utaenda kusaidia kupata vifaa vya maabara katika skuli hii ya Hasnuu Makame. Nasisitiza fedha hizi zitumike kwa uadilifu na umakini mkubwa ili kuhakikisha vifaa muhimu vinapatikana na wanafunzi wanapata fursa ya kujifunza kwa vitendo. Huu ni uwekezaji kwa wanafunzi … na taifa linawaangalia kama viongozi na wataalamu wa kesho," amesema Dkt. Mwanakhamis.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, amewasihi wanafunzi kusoma kwa juhudi na kuchangamkia fursa mbalimbali ambazo serikali inatoa kwao hasa kwa upande wa sayansi ikiwemo "Samia Scholarship", ambayo ni mahsusi kwa ajili ya wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika masomo sayansi kwenye mitihani ya kidato cha sita.

Makabidhiano hayo yameelezwa kuwa ni sehemu ya mkakati wa HESLB wa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuendeleza elimu nchini, ikiwa ni pamoja na kuchangia katika maboresho ya mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA), Dkt. Mwanakhamis Adam Ameir, ameongoza hafla ya makabidhiano ya TZS 10,000,000/= zilizotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara katika Shule ya Sekondari Hasnuu Makame, Mkoa wa Kusini Unguja.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyopambwa pia na burudani ya shairi mahsusi la tukio hilo, Dkt. Mwanakhamis ameishukuru HESLB kwa msaada huo na kusisitiza umuhimu wa matumizi sahihi ya fedha hizo kwa manufaa ya wanafunzi na walimu.

"Naishukuru HESLB kwa msaada huu ambao utaenda kusaidia kupata vifaa vya maabara katika skuli hii ya Hasnuu Makame. Nasisitiza fedha hizi zitumike kwa uadilifu na umakini mkubwa ili kuhakikisha vifaa muhimu vinapatikana na wanafunzi wanapata fursa ya kujifunza kwa vitendo. Huu ni uwekezaji kwa wanafunzi … na taifa linawaangalia kama viongozi na wataalamu wa kesho," amesema Dkt. Mwanakhamis.



# DC MKALIPA AZINDUA UTOAJI ELIMU YA UOMBAJI MKOPO 2025/2026

**MWANZA, JULAI 28, 2025**

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza, Mhe. Amir Mkalipa, ameongoza uzinduzi wa kitaifa wa zoezi la utoaji elimu kuhusu taratibu za uombaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2025/2026 uliofanyika Julai 28, 2025 katika ukumbi wa Rock City Mall na kushirikisha wadau mbalimbali wa elimu, wanafunzi, wazazi, watoa huduma za *internet cafes na stationaries.*

Akizungumza katika hafla hiyo ambayo wadau 1,012 walishiriki, Mhe. Mkalipa ambaye aliyekuwa mgeni rasmi akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtanda, alielezea fahari kwa Mkoa wa Mwanza kuwa mwenyeji na kinara wa uzinduzi huo muhimu kitaifa na kuwa miongoni mwa mikoa 22 ambayo Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ilipanga kufanya zoezi la kutoa elimu kuanzia Julai 28 hadi Agosti 10, 2025.

"Hii ni heshima kubwa kwetu na inaonesha jinsi ambavyo Mkoa wa Mwanza unatambulika katika juhudi zake za kuhimiza elimu na maendeleo ya watu wake," alisema Mhe. Mkalipa kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.

Katika hafla hiyo, Mhe. Mkalipa alieleza kuwa uzinduzi huo sio tu ni ishara ya kujivunia, bali pia ni jukwaa muhimu la kutoa maarifa kwa wanafunzi na wazazi kuhusu namna ya kuomba mikopo kwa usahihi ili kuhakikisha waombaji wahitaji wanafikiwa na kuwezeshwa, kwa kuwapangia mikopo ili kusoma vyuo vikuu. Alisisitiza na kutoa rai kwa wanafunzi, wazazi na walezi kujitokeza ili kupata elimu hiyo.

Aidha, katika hotuba yake, mgeni rasmi alieleza jinsi Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kuonesha dhamira ya dhati ya kuwekeza katika elimu ya juu. Alifafanua kuwa serikali imekuwa ikiongezea bajeti kila mwaka ili kuwafikia watanzania wengi zaidi.

"Kwa mwaka wa masomo ulioisha wa 2024/2025, bajeti ya mikopo ya elimu ya juu ilikuwa TZS 787 bilioni. Mwaka huu wa 2025/2026, bajeti hiyo imeongezeka na kufikia TZS 916 bilioni. Hili ni ongezeko kubwa linalolenga kuhakikisha kuwa watanzania wengi zaidi, hususan wale wa kipato cha chini, wanapata fursa ya kujiendeleza kielimu," alieleza Mhe. Mkalipa.

Licha ya kuzungumzia mikopo, Mhe. Mkalipa pia alizungumzia pia jitihada za Serikali kuanzisha 'Samia Scholarship' tangu mwaka wa masomo 2022/2023, ambayo inalenga kuwahamasisha wanafunzi wanaosoma tahasusi za Sayansi kufanya vizuri katika mitihani ya kidato cha sita inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA). Aidha, kuanzia mwaka wa masomo 2023/2024, Serikali imepanua wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa kuanza kuwakopesha wanafunzi wa ngazi ya Stashahada (Diploma).

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia alielezea umuhimu wa elimu hiyo kwa umma kuhusu taratibu za uombaji mkopo, kuwa huwasaidia wanafunzi na wazazi kuelewa vigezo, nyaraka muhimu na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kukamilisha maombi kwa usahihi.

Dkt. Kiwia aliwasihi wanafunzi, wazazi na walezi, pamoja na watoa huduma wa Internet Café na Stationeries, kushiriki kikamilifu kwenye zoezi hilo la utoaji wa elimu, kwa kuuliza maswali, kuchukua taarifa muhimu na kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma kwa kukosa taarifa sahihi kuhusu uombaji mikopo au 'Samia Scholarship'.

Mhe. Mkalipa alihitimisha hotuba yake kwa kuitaka HESLB pamoja na wadau wake ikiwemo Benki ya CRDB, kuhakikisha kuwa elimu ya uombaji mkopo

inakuwa endelevu na kuwafikia wananchi wengi zaidi katika mikoa yote nchini.

Uzinduzi huo, uliambatana na utoaji wa elimu na huduma za kifedha kwa wananchi ambapo pia wataalamu kutoka HESLB waliwasaidia wananchi kujua hatua za uombaji mkopo, namna ya kupata namba ya kumbukumbu kutoka mfumo wa anwani za makazi (NaPA) na kujibu maswali ya moja kwa moja kutoka kwa wananchi.

Wanafunzi kutoka shule za sekondari Nsumba, Ngaza, Taqwa, Bwiru (Wavulana), Bwiru (Wasichana), Buswelu (Wasichana), Holy Family (Wasichana), Mwanza, Loreto (Wasichana), Messa, Lake, Rorya, na Pamba, wanaomsoma tahasusi mbalimbali kidato cha tano na sita, walikuwa miongoni mwa washiriki.

Katika awamu hiyo ya kwanza ya uelimishaji kwa mwaka 2025/2026, elimu pia ilitolewa katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Pwani, Iringa, Morogoro, Unguja Kaskazini, Unguja Kusini, Mjini Magharibi, Pemba Kaskazini, Pemba Kusini, Mwanza, Kagera, Kigoma, Mbeya, Katavi, Njombe, Arusha, Tanga, Manyara, Mtwara, Ruvuma na Lindi

> **"Kwa mwaka wa masomo ulioisha wa 2024/2025, bajeti ya mikopo ya elimu ya juu ilikuwa TZS 787 bilioni. Mwaka huu wa 2025/2026, bajeti hiyo imeongezeka na kufikia TZS 916 bilioni. Hili ni ongezeko kubwa linalolenga kuhakikisha kuwa watanzania wengi zaidi, hususan wale wa kipato cha chini, wanapata fursa ya kujiendeleza kielimu,"**




# VIONGOZI WA ZHESLB WATEMBELEA HESLB

**DAR ES SALAAM, AGOSTI 1, 2025**
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZHESLB) Prof. Mohammed Hafidh akiambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZHESLB) Bi. Umrat Mohammed wametembelea Ofisi za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) zilizopo jijini Dar es Salaam.

Prof. Hafidh alifika kumtambulisha rasmi Mkurugenzi Mtendaji wa ZHESLB ambaye ameteuliwa kushika wadhifa huo na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, mwezi Machi mwaka huu.

Viongozi hao wawili wa ZHESLB walipokelewa na Menejimenti ya HESLB ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Bill Kiwia na kufanya mazungumzo kuhusu utendaji wenye tija wa taasisi hizo zinazoratibu ugharimiaji wa masomo kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu nchini kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar.

Taasisi hizo mbili zinazosimamia mikopo ya wanafunzi kwa upande wa Muungano (HESLB) na Zanzibar (ZHESLB) zimekuwa zikishirikiana kwa karibu kubadilishana ujuzi na uzoefu kwa lengo la kuboresha huduma kwa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu na ufanisi wa kiutendaji.



**Julai 08, 2025, Zanzibar:** Afisa Mikopo wa HESLB Bw.Juma Daudi Mlagala akitoa huduma kwa wanafunzi walioshiriki katika Wiki ya Elimu ya juu Zanzibar.



**Julai 08, 2025, Dar es salaam:** Afisa Mikopo Mwandamizi Bi. Deonista Komba akitoa elimu ya namna ya Uombaji Mikopo na Urejeshaji kwa baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Buyuni waliotembelea maonesho ya Sabasaba (DITF).



**Julai 28, 2025, Mwanza:** Picha ya pamoja ikiwaonesha baadhi ya wadau mbalimbali wa elimu waliohudhuria hafla ya ufunguzi wa mafunzo ya Uombaji mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka 2025/2026 yaliyofanyika katika ukumbi wa Rocky City Mall.



**Julai 27, 2025, Dodoma:** Baadhi ya watumishi wa HESLB wakiwa katika picha ya pamoja na Meneja wa HESLB wa kanda hiyo, Bi. Octavia Seleman (mwenye kofia ya ufito mwekundu) mara baada ya kushiriki mbio za hisani zilizoandaliwa na Benki ya NBC.



**Agosti 17, 2025, Dar es salaam:** Baadhi ya watumishi wa HESLB waliohudhuria mbio za hisani zilizoandaliwa na Benki ya CRDB, mbio hizo zilifanyika katika Viwanja vya Farasi jijini Dar es salaam.



Agosti 27, 2025, Dar es salaam: Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia (kulia) akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Mwanga Hakika, Bw. Jagjit Singh katika ofisi ya HESLB, Dar es salaam.




**Septemba 17, 2025, Dar es salaam:** Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia (katikati) akionesha ngao ya heshima aliyotunukiwa na Shule ya Sekondari Temeke mara baada ya sherehe za makabidhiano ya fedha za vifaa vya maabara, kulia ni Mkuu wa shule ya Temeke Bi. Ingia Madika Mtenga na kushoto ni dada mkuu wa shule hiyo Clara Victor Kisanga.




**Septemba 25, 2025, Belgium:** Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia (katikati) alibadilishana mawazo na baadhi wa watanzania wanufaika wa mkopo wa elimu ya juu walioshiriki tamasha la michezo (Serengeti bonanza) lililofanyika katika jiji la Antwerp.




**Septemba 17, 2025, Zanzibar:** Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA), Dkt. Mwanakhamis Adam Ameir (katikati) akiongoza makabidhiano ya mfano wa hundi yenye thamani ya shilingi milioni kumi (10,000,000) kwa Shule ya Sekondari Hasnuu Makame. Kulia kwa Dkt. Mwanakhamis ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia.




# DKT. KIWIA ATOA HUDUMA MAONESHO WIKI YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR

**Maonesho ya Sita ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar yalianza tarehe 14 Julai, 2025 na kuhitimishwa tarehe 20 Julai 2025 katika viwanja vya Mnazi Mmoja vilivyoko Mkoa wa Mjini Magharibi.**

**ZANZIBAR, JULAI 19, 2025**
Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia, Jumamosi ya tarehe 19 Julai, 2025 alishiriki kikamilifu kutoa huduma na elimu kwa wananchi kuhusu utoaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu katika Maonesho ya Sita ya Wiki ya Elimu ya Juu yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja vilivyoko Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Pamoja na kutoa huduma katika banda la HESLB, Dkt. Kiwia alisisitiza umuhimu wa wanafunzi na wazazi kuelewa taratibu za kuomba mikopo, namna ya kufanya malipo vyuoni, na wajibu wa kurejesha mikopo kwa wakati kutoka kwa wanufaika waliohitimu.

Kupitia banda la HESLB, wananchi walipata fursa ya kuuliza maswali, kupata maelezo, ufafanuzi wa kina na kujifunza kuhusu jinsi ya kutumia mfumo wa maombi ya mikopo kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

Aidha, katika maonesho hayo, HESLB iliendeleza ushirikiano wa karibu na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kutoa elimu juu ya matumizi ya Anwani ya Makazi (NaPA), ambayo ni moja ya vipengele muhimu katika mchakato wa maombi ya mikopo. Ushirikiano huu unalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wenye sifa wanaoomba mikopo wanapata huduma kwa usawa na ufanisi.

Katika kuendeleza uhusiano na wadau wa elimu ya juu, Dkt. Kiwia alipata wasaa wa kutembelea mabanda mbalimbali, likiwemo la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZHESLB) ambapo alijadiliana na viongozi wa taasisi hiyo kuhusu masuala ya ushirikiano, kubadilishana uzoefu, na kuboresha mifumo ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa pande zote mbili za Muungano.

Ushiriki wa HESLB kwenye Maonesho ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar, ni sehemu ya juhudi za kuendeleza uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa mikopo, sambamba na kuhamasisha urejeshaji wa mikopo ili kuwezesha wanafunzi wahitaji kupata fursa ya kugharimiwa masomo yao ya elimu ya juu.

Maonesho ya Sita ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar yalianza tarehe 14 Julai, 2025 na kuhitimishwa tarehe 20 Julai 2025 katika viwanja vya Mnazi Mmoja vilivyoko Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo zaidi ya wageni 2,000 walitembelea na kupata huduma katika banda la HESLB.




# WIKI YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR

**ZANZIBAR- JULAI 17, 2025**
Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Mhe. Lela Muhamed Mussa amefungua rasmi Maonesho ya Sita ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar mnamo Julai 17, 2025 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Mkoa wa Mjini Magharibi na kutembelea Banda la HESLB.

Kabla ya hafla ya kufungua maonesho, Mhe. Waziri Lela alipongeza kazi nzuri inayofanywa na HESLB kwenye utoaji wa elimu kuhusu utaratibu wa kuomba mikopo, taratibu za malipo vyuoni na urejeshaji wa mikopo.

Aidha, Mhe. Waziri alionesha kuvutiwa na ushirikiano baina ya HESLB na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika kuhakikisha wanafunzi wanapata huduma ya kufundishwa jinsi ya kupata namba za anwani za makazi (NaPA) kwa ajili ya kutumika kama sehemu muhimu ya taarifa za maombi ya mikopo kwa mwaka 2025/2026.

“Hii ni njia sahihi ya kuwasaidia wadau na hasa wanafunzi hawa ambao wanaomba mikopo kipindi hiki wakijiandaa kujiunga na vyuo”, alisema Waziri Lela.

Kwa upande wa Pemba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) Zanzibar, Ndugu Khamis Abdullah Said alifungua rasmi Maonesho ya Tatu ya Wiki ya Elimu ya Juu tarehe 24 Julai, 2025 katika Viwanja vya Gombani.

Akiwa katika banda la HESLB, Katibu Mkuu alisisitiza umuhimu wa HESLB kuendelea kuboresha na kurahisisha huduma kwa wanafunzi wanaoomba mikopo na kushirikiana na wadau wake wa kimkakati ili kuwawezesha waombaji mikopo kupata nyaraka muhimu na kukamilisha maombi ya mikopo kwa wakati.

“…Nyie ni watu muhimu sana katika kuwawezesha watanzania kufikia malengo yao, hakikisheni kwa kushirikiana na wadau wenu mnawawezesha waombaji mikopo kupata nyaraka zinazohitajika kwa wakati ili wanafunzi wakamilishe maombi yao ya mikopo katika muda uliopangwa”, alisisitiza Katibu Mkuu wa WEMA.

Katika maonesho hayo, HESLB ilitoa huduma kwa wanafunzi waombaji mikopo, wazazi, walezi, wadau wa elimu na wananchi kwa ujumla waliofika kwenye maonesho hayo na akutembelea banda la Bodi ya Mikopo.

HESLB imekuwa ikishiriki katika Maonesho ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar tangu yalipoanzishwa mwaka 2020 ili kutoa huduma za utoaji na urejeshaji mikopo sambamba na kuhabarisha umma kuhusu masuala mbalimbali ya HESLB.



CAREBO

# HESLB imenivusha

## Mhitimu wa Shahada ya Uhasibu Chuo cha Uhasibu Mbeya

**Iringa, Septemba 09, 2025**

Maisha ni mwalimu bora. Ni msemo ambao Carebo Peter Malogage, kijana mwenye umri wa miaka 25 kutoka kijiji cha Kilolo mkoani Iringa, anaweza kuuthibitisha kwa ujasiri. Leo hii anasimama kama mhitimu wa shahada ya Uhasibu kutoka Chuo cha Uhasibu (TIA), Kampasi ya Mbeya. Hata hivyo, safari ya Carebo kufikia hapa haikuwa rahisi.

Akisimulia historia ya elimu na maisha yake katika mahojiano maalumu na HESLB Yako, Carebo anafunguka kwa hisia akisema: "HESLB imenivusha. Bila mkopo wa elimu ya juu, ndoto zangu zingeishia njiani."

**Changamoto za Elimu ya Sekondari**

Safari ya Carebo kielimu haikuwa ya kifahari, baada ya kumaliza kidato cha nne, alijiunga na Shule ya Sekondari Matamba kwa masomo ya kidato cha tano na sita. Anasema, katika hatua hiyo ya elimu ndipo maisha yalipoanza kumjaribu zaidi, ada za shule zilikuwa mzigo mzito kwa familia yao yenye watoto watano, na mara kadhaa alilazimika kukaa nyumbani akingoja wazazi wake wakusanye fedha za kutosheleza kulipa ada.

"Kulikuwa na nyakati nilihisi kukata tamaa kabisa," anakumbuka Carebo kwa sauti yenye hisia na kuongeza, "… nilifikia hatua ya kufikiria kuacha shule, lakini nikajipa moyo kwamba siku hazigandi. Nikajua nikijitahidi, nitafika tu."

Wazazi wake, Bw. na Bi. Peter Malogage, ni watu wa kipato cha chini waliokuwa wakijitahidi kuwasomesha watoto wao wote watano, changamoto ya kugawa kipato chao kidogo kwa watoto waliokuwa shule kwa nyakati zinazokaribiana haikuwa jambo dogo.

**Ndoto Zainuliwa na Mkopo wa Elimu**

…baada ya kumaliza kidato cha sita, Carebo alipata nafasi ya kujiunga na Chuo cha Uhasibu (TIA), kampasi ya Mbeya kusomea Shahada ya Uhasibu. Hapo ndipo ndoto yake ilianza kuchanua kwa msaada wa mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

"Kama si mkopo huu, maisha yangekuwa gizani," anasema Carebo kwa msisitizo.

"Familia yangu isingeweza kumudu gharama za masomo, malazi na chakula kwa miaka yote mitatu ya chuo. Lakini HESLB ilinifanya nikae darasani kwa amani na kuwekeza nguvu zangu zote kwenye masomo."

**Kujiajiri Kupitia Teknolojia**

Leo hii, Carebo si tu mhitimu bali pia ni mjasiriamali wa mitandaoni, amejikita katika kutoa elimu na usaidizi kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati, hususan katika kuagiza bidhaa mitandaoni na kupata wateja kupitia majukwaa ya kidigitali.

"Nilijua mapema kuwa maisha baada ya chuo yanahitaji ubunifu, hivyo niliamua kuwekeza maarifa yangu kwenye teknolojia na biashara mtandaoni. Sasa ninaelimisha watu namna ya kutumia mtandao kukuza biashara zao." anasema Carebo,

**Ushauri kwa Wanafunzi Waliopo Vyuo Vikuu**

Carebo ana wito maalumu kwa wanafunzi walioko vyuoni:

- Jifunzeni elimu ya fedha – kuelewa namna ya kutunza na kubajeti fedha kutawasaidia kupunguza changamoto za kifedha baada ya kuhitimu.
- Tambueni kuwa fedha mnazopata kutoka HESLB ni mkopo – si zawadi; ni mkopo. Kwa hiyo, anawasihi wahitimu wote kuanza kurejesha mikopo yao mara baada ya kuanza kujipatia kipato.

"Mtu akijua thamani ya fedha na wajibu wake, maisha huwa rahisi na yenye mipangilio mizuri," anasisitiza Carebo.

Kutoka kijijini Kilolo, kijana huyu mdogo wa mwisho katika familia ya watoto watano amepambana, amevumilia na sasa anavuna matunda ya bidii yake. Hadithi ya Carebo Peter Malogage ni ushahidi wa nguvu ya matumaini, elimu na msaada wa taasisi zinazowawezesha vijana kufanikisha ndoto zao.

"Kama nimeweza kufanikisha ndoto zangu licha ya changamoto zote, basi naamini kila kijana anaweza. Siku hazigandi. Pambana kijana usikate tamaa," anahitimisha Carebo kwa tabasamu.



# BARAZA LA WAFANYAKAZI HESLB LAKUTANA MOROGORO

### Lajadili maboresho ya utendaji na utatuzi wa changamoto za wafanyakazi

**Morogoro, Ijumaa, Septemba 12, 2025**
Baraza la Wafanyakazi la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) limekutana Septemba 12, 2025 mjini Morogoro kujadili masuala mbalimbali yanayolenga kuboresha utendaji kazi wa taasisi hiyo, huku Menejimenti ikitoa majibu ya hoja mbalimbali zilizotolewa na wajumbe wa baraza hilo.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia ambaye ndiye Mwenyekiti wa Baraza hilo, alisema Baraza la Wafanyakazi ni chombo muhimu kinachosaidia kuongeza uwajibikaji na ushirikiano kati ya Menejimenti na watumishi.

"Kupitia Baraza la Wafanyakazi tunapata mrejesho wa moja kwa moja kutoka kwa watumishi wetu. Hii inatupa fursa ya kutatua changamoto zao na kuweka mikakati ya kuongeza ufanisi," alisema Dkt Kiwia.

Kwa upande wake, mmoja wa wajumbe wa baraza, Bi. Dorah Konga, alipoongea na HESLB Yako alisema baraza limekuwa msaada mkubwa katika kuhakikisha sauti za watumishi zinasikika kwa Menejimenti.

"Hii ni nafasi ya kipekee kwa sisi wafanyakazi kueleza changamoto zetu na kutoa mapendekezo ili kuboresha mazingira ya kazi. Tunashukuru kwa majibu na hatua zinazochukuliwa na Menejimenti," amesema Bi. Dorah.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Habari, Ufundi Stadi na Utafiti (RAAWU), Tawi la HESLB, Bw. Daud Elisha alibainisha kuwa majadiliano ya kina kwenye Baraza la Wafanyakazi ni muhimu sana kwa kuwa yanagusa maslahi ya watumishi na kuboresha mazingira yao ya kazi.

"Maslahi na mazingira bora ya kazi ni kichocheo cha kuongeza tija na ufanisi katika kazi za taasisi. Tumetoa maoni kadhaa ambayo Menejimenti imeahidi kuyafanyia kazi," amesema Bw. Elisha.

Baraza la Wafanyakazi ni jukwaa muhimu la kiutendaji linalowawezesha watumishi kushiriki katika maamuzi ya kitaasisi. Kwa mujibu wa Menejimenti ya HESLB, chombo hicho kimeendelea kuwa nguzo ya mshikamano, uelewano na ari ya kufanya kazi kwa pamoja baina ya Menejimenti na watumishi katika kutimiza majukumu ya kitaasisi.

# WASILIANA NASI:

## DODOMA

Jengo la PSSSF,
Br. Makole, eneo la
Uhindini
S.L.P 984, Dodoma
Simu +255 758 067577
+255 739 06757
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## ARUSHA

NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712,Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Barua Pepe:
arusha@heslb.go.tz

## MWANZA

PSSSF Plaza, ghorofa
ya pili Br. Kenyatta
S.L.P 3051, Mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Barua Pepe:
mwanza@heslb.go.tz

## ZANZIBAR

Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900, Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Barua Pepe:
zanzibar@heslb.go.tz

## HUDUMA KWA WATEJA

PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068, Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## MBEYA

Jengo la CAG, Ghorofa ya
Nne, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Barua Pepe:
mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA

NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya tatu,
Kitalu Na. 217, Block H, Karibu
na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P: 969, Mtwara.
Simu: +255 733 068 171
Barua Pepe:
mtwara@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM

Bodi ya Mikopo ya
Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
1 Mtaa wa Kilimo,Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068,
15471-Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz